SCCULT (1992) LIMITED

The Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania (1992) Limited P.O. Box 20640- email: info@sccult.tz,Website:www.sccult.tz TEL. +255 222 185 548/9
Ushirika Tower Lumumba Street, 16 Floor – DAR ES SALAAM – TANZANIA

SCCULT/GNRL/VOL.I/036 **OKTOBA 26, 2026.**

VIONGOZI, WATENDAJI, WANACHAMA NA WADAU,
VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS),
TANZANIA-BARA.

YAH: MWALIKO WA KUSHIRIKI KONGAMANO LA MWISHO WA MWAKA KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO (SACCOS)-TANZANIA (TANZANIA SACCOS ANNUAL SUMMIT 2026), MOROGORO, TAREHE 30 NOVEMBA HADI 2 DISEMBA 2026.

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu;

1. SCCULT (1992) Ltd kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) tunapenda kuwaalika Viongozi, watendaji, wanachama na wadau wote wa maendeleo kushiriki kwenye Kongamano Maalumu la mwisho wa mwaka Tanzania 2026 (Tanzania SACCOS Annual Summit 2026), litakaofanyika Morogoro kuanzia tarehe 30 Novemba hadi 2 Disemba 2026.
2. Kongamano hili litafanyika chini ya kaulimbiu isemayo:
   "Kujenga SACCOS Imara, Himilivu na Endelevu kwa Maendeleo jumuishi ya Kiuchumi."
3. Kongamano hili linafanyika kufuatia mafanikio makubwa ya SACCA Congress 2026, iliyofanyika kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania na kushirikisha taasisi zaidi ya 350 kutoka nchi 28, pamoja na washiriki takribani 1,300. SCCULT (1992) Ltd ilikuwa mwenyeji na mhimili wa uratibu wa kongamano hilo muhimu la Kimataifa.
4. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo gharama za ushiriki, baadhi ya SACCOS na vyama vingine vya ushirika havikuweza kushiriki katika kongamano hilo. Kwa kutambua umuhimu wa kuhakikisha kuwa

Sekta nzima inanufaika na matokeo, uzoefu na maarifa yaliyopatikana, SCCULT (1992) Ltd na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) tumeona umuhimu wa kuandaa Kongamano hili la Kitaifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa, kujadili maendeleo ya Sekta na kuweka Mikakati ya pamoja ya kuimarisha Ushirika wa Akiba na Mikopo Nchini.

5. Kongamano hili litatoa fursa ya kujadili Taarifa ya Utendaji wa SACCOS ya mwaka 2025, kutathmini mafanikio na changamoto za Sekta, kubadilishana uzoefu na kuweka Mikakati ya kuimarisha utawala bora, uendelevu wa kifedha, ubunifu, matumizi ya teknolojia na utoaji wa huduma bora kwa wanachama.
6. Miongoni mwa masuala yatakayojadiliwa ni:
    i. Mrejesho wa matokeo, mafunzo na mapendekezo muhimu kutoka SACCA Congress 2026;
    ii. Uwasilishaji na majadiliano kuhusu Taarifa ya Utendaji wa SACCOS ya mwaka 2025;
    iii. Kuimarisha uongozi, utawala bora, uwajibikaji na usimamizi wa vihatarishi katika Ushirika wa Akiba na Mikopo;
    iv. Ubunifu, matumizi ya teknolojia na mikakati ya kuboresha huduma kwa wanachama.
    v. Kubadilishana uzoefu na mbinu bora za kuimarisha utendaji na uendelevu wa Ushirika wa Akiba na Mikopo;
    vi. Kuendeleza mshikamano na maadili ya ushirika, sambamba na kutambua ari ya Siku ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani (International Credit Union Day) ya mwaka 2026.

7. ADA YA USHIRIKI NA USAJILI:

Ada ya ushiriki katika Kongamano hili ni TZS. 400,000/= (Laki nne tu) kwa mshiriki mmoja kwa SACCOS na TZS. 500,000 (Laki tano tu) kwa taasisi zisizokuwa SACCOS. Malipo ya ada yafanyike kupitia Account hii; ***SCCULT EDUCATION FUND A/C No. 01J1007424900, CRDB – LUMUMBA BRANCH.***

Usajili utaanza rasmi tarehe 01 Novemba 2026 na kufungwa tarehe 20 Novemba 2026. SACCOS/Taasisi zinazoalikwa

zinahimizwa kusajili washiriki wao ndani ya muda uliopangwa kwa kutumia link hii https://events.sccult.tz ili kurahisisha maandalizi na uratibu wa Kongamano hili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu usajili na ushiriki, tafadhali wasiliana na:

i. Leah D. Mbilinyi 0768 917 743 AU baruapepe leah.daudi@sccult.tz
ii. Gloria Anthony 0672 035 453 AU baruapepe glory.anthony@sccult.tz

8. Aidha kutakuwa na utaratibu wa ushiriki wa wadhamini ambao watakuwa tayari kushirikiana nasi kwenye Kongamano hili na taarifa zaidi zitatolewa na Maafisa ambao mawasiliano yao yametolewa hapo juu.
9. Tunaamini kuwa ushiriki wenu utachangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya Kongamano hili na kujenga msingi imara wa ushirikiano, uwajibikaji na Maendeleo endelevu ya SACCOS na Vyama vingine vya Ushirika Nchini Tanzania.
10. Tunawakaribisha Morogoro.
11. ***Pamoja na Salamu za SACCOS.***

Hassani S. Mnyone (ADE)
KATIBU MTENDAJI.

SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE UNION
P. O. Box 20640
DAR ES SALAAM
LEAGUE OF TANZANIA (1992) LTD.

NAKALA:

1. TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA,
   MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA,
   S.L.P 201, DODOMA,
   TANZANIA.

2. TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA,
   MRAJIS MSAIDIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA MKOA WA MOROGORO,
   TANZANIA.

3. WARAJIS WASAIDIZI WA MIKOA YOTE,
   TANZANIA-BARA.

4. MKURUGENZI MTENDAJI,
   SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO),
   S.L.P 761, DODOMA,
   TANZANIA.

5. MKURUGENZI MTENDAJI,
   SHIRIKISHO LA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA (TFC),
   S.L.P 2567, DAR ES SALAAM,
   TANZANIA.

6. MAKAMU MKUU WA,
   CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MoCU),
   S.L.P 474, MOSHI-KILIMANJARO,
   TANZANIA.